

**BIBLIA KWA TASWIRA, AJGANO JIPYA, KITABU CHA 27
WAGALATIA, Sehemu ya Pili**

SHERIA NA NEEMA

(VISUALIZED BIBLE, Vol 27, N.T. Law and Grace)

Mwandishi: Marilyn L. Habecker

Muchapaji: Frances H. Hertzler

Imegeuzwa kwa Swahili Congo na watumishi wa Mungu katika DR Congo

©1972 Bible Visuals International

PO Box 153, Akron, PA 17501-0153

Telephone: 717-859-1131 Fax: 717-859-4360

www.biblevisuals.org

SOMO 1 – SHERIA NI NINI ?

Kwa Mwalimu kujifunza mbele : Wagalatia, sura 3. Kutoka 20:1 hadi 24:11. Walawi sura 16.

Shabaa ya somo: Kuonyesha kwamba sheria ilikuwa vizuri lakini haikuokoa watu.

Yale ambayo wanafunzi wako wangelipaswa kujua: Sheria ilikuwa mwongozi wa Waisraeli mpaka kuja kwa Kristo mara ya kwanza.

Yale ambayo wanafunzi wako wangelipaswa kutambua: Kushukuru Mungu kwa sababu hakuwakaza kushika sheria kusudi wawe wake.

Yale ambayo wanafunzi wako wangelipaswa kufanya: Wasioamini : Kujitoa kabisa kwa Kristo kama Bwana na Mukozi wao. Walioamini : Kuomba Mungu awapatie wakati katika juma huu kuonyesha njia ya kwali ya kufika mbinguni kwa asiyejua njia.

Somo kwa kifupi (Kwandika katika buku la mwalimu na la wanafunzi):

1. Mungu aliwapa Waisraeli sheria kuwafunulia maana ya zambi (Wagalatia 3 :10, 19, 22.)
2. Katika sheria Mungu alitoa utaratibu wa sadaka kwa kufunika zambi.
3. Hukumu ya kuasi sheria ilikuwa kufa (Wagalatia 3.10.) 4. Sheria ilifanya kazi ya kuongoza watu mupaka Kristo alipokufa (Wagalatia 3 :24-25.)

Shairi la kujua kwa ufahamu: Wagalatia 3:13 – Kristo alitukomboza kwa laana ya torati, akikuwa alifanywa laana kwa ajili yetu. (Maana ya "kufanya laana", Kristo alikufa kwa pahali petu.)

Maelezo kwa Mwalimu :

Wagalatia ni kitabu kikubwa katika Agano Jipya. Tushukuru Mungu kila mara kwa barua hii nzuri. Kama Paulo asingalionyesha Wagalatia makosa yao (ya kufuata mafundisho ya uwongo), kweli ya Habari Njema ya Kristo ingalipotea katika inchi ile. Mungu alitumika kwa njia ya Paulo kulinda kweli ile.

Katika sura ya kwanza na ya pili ya Wagalatia tuliona kwamba waamini wale walikuwa wameanza kuwa na shaka juu ya mafundisho ya Paulo aliyesema wokovu unapatikana kwa njia ya imani katika Kristo pasipo kitu kingine. Walikuwa na shaka kwa sababu walimu wa uwongo walibisha cheo chake kama mutume. Kwa hivi katika Wagalatia sura 1 na 2 Paulo alihakikisha kuitwa na Mungu kwake. Kwa sura 3 na 4 Paulo anasimamia Habari Njema. Ndani ya masomo ya sasa tutajifunza mambo ya sheria na neema. itasaidia watoto kama watasoma Wagalatia 3 na 4 kwao wakati tunapoendelea na masomo haya.